

**KUMB: PPR/19 - 03/1**

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 6 MACHI 2019**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 6 Machi 2019**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote (Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa) yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam, zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 6 Februari 2019. Kwa mwezi Machi 2019, bei za rejareja za Petroli zimepungua kwa Shilingi 23/lita (sawa na asilimia 1.07) wakati bei za Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 51/lita (sawa na asilimia 2.44) na Shilingi 50/lita (sawa na asilimia 2.47), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli zimepungua kwa Shilingi 22.68/lita wakati zile za Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 50.68/lita (sawa na asilimia 2.59) na Shilingi 50.30/lita (sawa na asilimia 2.62), mtawalia. Kwa kiasi kikubwa, mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la ndani kwa mafuta yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam yanatokana na mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la dunia pamoja na gharama za usafarishaji (*BPS Premium*) kama inavyoonekana katika **Jedwali C**.
- (b) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Tanga zimepungua ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 6 Februari 2019. Bei za Mafuta ya Taa hazijabadilika kwa sababu hakuna shehena ya bidhaa hiyo iliyopokelewa nchini kupitia bandari ya Tanga kwa mwezi wa Februari 2019. Kwa mwezi Machi 2019, bei za rejareja za Petroli na Dizeli **kwa Mikoa ya Kaskazini** zimepungua kwa Shilingi 64/lita (sawa na asilimia 2.91) na Shilingi 104/lita (sawa na asilimia 4.65), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimepungua kwa Shilingi 63.86/lita (sawa na asilimia 3.08) na Shilingi 103.86/lita (sawa na asilimia 4.90), mtawalia. Kwa kiasi kikubwa, mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la ndani kwa mafuta yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Tanga kunatokana na mabadiliko ya bei za mafuta hayo katika soko la dunia kama inavyoonekana katika **Jedwali C**.
- (c) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Mtwara zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 6 Februari 2019. Kwa mwezi Machi 2019, bei za rejareja za Petroli na Dizeli **kwa Mikoa ya Kusini** zimeongezeka kwa Shilingi 31/lita (sawa na asilimia 1.50) na Shilingi 147/lita (sawa na asilimia 7.09), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa Shilingi 31.32/lita (sawa na asilimia 1.59) na Shilingi 146.73/lita (sawa na asilimia 7.52), mtawalia. Kwa kiasi kikubwa, mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la ndani kwa mafuta yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Mtwara yanatokana na mabadiliko ya bei za mafuta hayo katika soko la dunia na kuongezeka kwa gharama za usafirishaji (*BPS premiums*).

- (d) Ifahamike kuwa, tofauti za mabadiliko ya bei za mafuta kati ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara inatokana na tofauti ya bei zilizotumika kukokotoa bei hizo za mafuta kwa sababu ya tofauti za miezi ya kuingizwa mafuta nchini kupitia bandari hizo tatu pamoja na tofauti ya gharama za usafirishaji (*BPS Premium*) kwenye bandari hizo tatu.
- (e) EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba **\*152\*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (f) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (g) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (*price cap*) kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula*) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 163 la mwezi Aprili 2018 na Gazeti la Serikali Na. 269 la mwezi Juni 2018.****
- (h) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (i) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

### JEDWALI A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
<b>Dar es Salaam</b>	<b>2,098</b>	<b>2,131</b>	<b>2,096</b>
<b>Arusha</b>	<b>2,191</b>	<b>2,195</b>	<b>2,286</b>
Arumeru (Usa West)	2,191	2,195	2,286
Karatu	2,209	2,213	2,304
Longido	2,202	2,206	2,297
Monduli	2,196	2,200	2,291

Monduli-Makuyuni	2,201	2,205	2,296
Ngorongoro (Loliondo)	2,276	2,280	2,371
<b>Pwani (Kibaha)</b>	<b>2,102</b>	<b>2,135</b>	<b>2,101</b>
Bagamoyo	2,109	2,142	2,107
Chalinze Junction	2,112	2,145	2,111
Chalinze (Msata)	2,116	2,149	2,115
Kibiti	2,118	2,151	2,117
Kisarawe	2,105	2,138	2,104
Mkuranga	2,108	2,140	2,106
Rufiji	2,125	2,158	2,124
<b>Dodoma</b>	<b>2,157</b>	<b>2,189</b>	<b>2,155</b>
Bahi	2,164	2,197	2,162
Chamwino	2,152	2,185	2,150
Chemba	2,183	2,216	2,182
Kondoa	2,189	2,222	2,188
Kongwa	2,154	2,187	2,152
Mpwapwa	2,158	2,191	2,156
Mtera (Makatopora)	2,175	2,208	2,174
<b>Geita</b>	<b>2,263</b>	<b>2,296</b>	<b>2,262</b>
Bukombe	2,252	2,285	2,251
Chato	2,284	2,317	2,283
Mbogwe	2,301	2,334	2,300
Nyang'hwale	2,278	2,311	2,277
<b>Iringa</b>	<b>2,162</b>	<b>2,195</b>	<b>2,161</b>
Ismani	2,167	2,200	2,166
Kilolo	2,166	2,199	2,165
Mufindi (Mafinga)	2,172	2,205	2,171
<b>Kagera (Bukoba)</b>	<b>2,313</b>	<b>2,346</b>	<b>2,312</b>
Biharamulo	2,288	2,320	2,286
Karagwe (Kayanga)	2,330	2,363	2,328
Kyerwa (Ruberwa)	2,335	2,368	2,334
Muleba	2,313	2,346	2,312
Ngara	2,301	2,334	2,300
Misenyi	2,322	2,355	2,320
<b>Katavi (Mpanda)</b>	<b>2,306</b>	<b>2,339</b>	<b>2,304</b>
Mlele (Inyonga)	2,288	2,320	2,286
Mpimbwe (Majimoto)	2,298	2,331	2,297
<b>Kigoma</b>	<b>2,329</b>	<b>2,362</b>	<b>2,328</b>
Uvinza (Lugufu)	2,341	2,374	2,340
Buhigwe	2,318	2,351	2,317
Kakonko	2,286	2,319	2,285
Kasulu	2,315	2,348	2,314
Kibondo	2,293	2,326	2,292
<b>Kilimanjaro (Moshi)</b>	<b>2,181</b>	<b>2,185</b>	<b>2,276</b>
Hai (Bomang'ombe)	2,184	2,188	2,279
Mwanga	2,174	2,178	2,269
Rombo (Mkuu)	2,197	2,201	2,292
Same	2,167	2,171	2,262

Siha (Sanya Juu)	2,187	2,191	2,282
<b>Lindi</b>	<b>2,141</b>	<b>2,236</b>	<b>2,155</b>
Lindi-Mtama	2,146	2,240	2,173
Kilwa Masoko	2,165	2,259	2,130
Liwale	2,177	2,271	2,176
Nachingwea	2,161	2,256	2,185
Ruangwa	2,167	2,262	2,186
<b>Manyara (Babati)</b>	<b>2,225</b>	<b>2,229</b>	<b>2,320</b>
Hanang (Katesh)	2,236	2,240	2,331
Kiteto (Kibaya)	2,240	2,244	2,335
Mbulu	2,238	2,242	2,333
Simanjiro (Orkasumet)	2,257	2,261	2,352
<b>Mara (Musoma)</b>	<b>2,276</b>	<b>2,309</b>	<b>2,275</b>
Musoma Vijijini (Busekela)	2,317	2,350	2,316
Rorya (Ingirijuu)	2,285	2,318	2,284
Rorya (Shirati)	2,320	2,353	2,319
Bunda	2,268	2,300	2,266
Butiama	2,273	2,306	2,272
Serengeti (Mugumu)	2,322	2,355	2,321
Tarime	2,287	2,320	2,286
Tarime (Kewanja/Nyamongo)	2,292	2,325	2,291
<b>Mbeya</b>	<b>2,205</b>	<b>2,238</b>	<b>2,204</b>
Chunya	2,214	2,247	2,213
Chunya (Makongolosi)	2,229	2,262	2,227
Kyela	2,221	2,254	2,219
Mbarali (Rujewa)	2,189	2,222	2,188
Rungwe (Tukuyu)	2,214	2,247	2,213
<b>Morogoro</b>	<b>2,123</b>	<b>2,156</b>	<b>2,121</b>
Mikumi	2,138	2,171	2,137
Kilombero (Ifakara)	2,161	2,194	2,159
Kilombero (Mlimba)	2,183	2,216	2,182
Kilombero (Mngeta)	2,172	2,205	2,171
Ulanga (Mahenge)	2,171	2,204	2,170
Malinyi	2,182	2,214	2,180
Kilosa	2,141	2,174	2,140
Gairo	2,141	2,174	2,140
Mvomero (Wami Sokoine)	2,133	2,166	2,132
Turiani	2,148	2,181	2,146
<b>Mtwara</b>	<b>2,127</b>	<b>2,222</b>	<b>2,169</b>
Nanyumbu (Mangaka)	2,164	2,258	2,218
Masasi	2,144	2,238	2,195
Newala	2,148	2,243	2,201
Tandahimba	2,141	2,236	2,194
Nanyamba	2,141	2,236	2,194
<b>Mwanza</b>	<b>2,248</b>	<b>2,281</b>	<b>2,247</b>
Kwimba	2,266	2,299	2,264
Magu	2,256	2,289	2,255
Misungwi	2,242	2,275	2,241

Sengerema	2,280	2,313	2,279
Ukerewe	2,307	2,340	2,306
<b>Njombe</b>	<b>2,190</b>	<b>2,223</b>	<b>2,189</b>
Njombe (Kidegembye)	2,211	2,244	2,209
Ludewa	2,228	2,261	2,227
Makambako	2,182	2,215	2,181
Makete	2,221	2,254	2,220
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,188	2,221	2,187
<b>Rukwa (Sumbawanga)</b>	<b>2,271</b>	<b>2,304</b>	<b>2,269</b>
Sumbawanga Rural (Mtowisa)	2,271	2,304	2,269
Kalambo (Matai)	2,278	2,311	2,277
Nkasi (Namanyeke)	2,284	2,317	2,283
<b>Ruvuma (Songea)</b>	<b>2,213</b>	<b>2,308</b>	<b>2,220</b>
Mbinga	2,226	2,320	2,253
Namtumbo	2,204	2,299	2,249
Nyasa (Mbamba Bay)	2,251	2,346	2,264
Tunduru	2,178	2,273	2,279
<b>Shinyanga</b>	<b>2,227</b>	<b>2,260</b>	<b>2,225</b>
Kahama	2,240	2,273	2,239
Kishapu	2,255	2,288	2,254
Ushetu (Nyamilangano)	2,258	2,291	2,257
Simiyu (Bariadi)	2,268	2,301	2,267
Busega (Nyashimo)	2,261	2,294	2,260
Itilima (Lagangabilili)	2,271	2,304	2,270
Maswa	2,260	2,293	2,258
Meatu (Mwanhuzi)	2,267	2,300	2,265
<b>Singida</b>	<b>2,188</b>	<b>2,221</b>	<b>2,187</b>
Iramba	2,201	2,234	2,199
Manyoni	2,173	2,206	2,172
Ikungi	2,184	2,217	2,183
Mkalama (Nduguti)	2,213	2,246	2,212
<b>Songwe (Vwawa)</b>	<b>2,214</b>	<b>2,247</b>	<b>2,213</b>
Songwe (Mkwajuni)	2,221	2,254	2,220
Ileje	2,218	2,251	2,217
Momba (Chitete)	2,223	2,256	2,222
Tunduma	2,218	2,251	2,217
<b>Tabora</b>	<b>2,252</b>	<b>2,285</b>	<b>2,251</b>
Igunga	2,206	2,239	2,205
Kaliua	2,271	2,304	2,270
Ulyankulu	2,265	2,298	2,264
Nzega	2,217	2,249	2,215
Sikonge	2,264	2,297	2,262
Urambo	2,265	2,298	2,264
Uyui	2,253	2,286	2,252
<b>Tanga</b>	<b>2,134</b>	<b>2,138</b>	<b>2,229</b>
Handeni	2,155	2,159	2,250
Kilindi	2,170	2,174	2,265
Korogwe	2,146	2,151	2,241

Lushoto	2,156	2,160	2,251
Mkinga (Maramba)	2,141	2,145	2,236
Muheza	2,139	2,143	2,234
Pangani	2,141	2,145	2,236

### JEDWALI B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla - DSM	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	1,974.16	2,006.58	1,973.03

Bei za Jumla - TANGA	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,010.62	2,014.35	2,105.56

Bei za Jumla - MTWARA	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,003.80	2,097.85	-----

### JEDWALI C: SABABU ZA MABADILIKO YA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI

#### BANDARI YA DAR ES SALAAM

	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia	Punguzo la Dola 23.601/Tani	Ongezeko la Dola 15.017/Tani	Ongezeko la Dola 0.944/Tani
Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (BPS premiums)	Ongezeko la Dola 6.663/Tani	Punguzo la Dola 4.423/Tani	Ongezeko la Dola 4.470/Tani

#### BANDARI YA TANGA

	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia	Punguzo la Dola 69.511/Tani	Punguzo la Dola 80.197/Tani	----
Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (BPS premiums)	Punguzo la Dola 1.880/Tani	Punguzo la Dola 1.120/Tani	----

#### BANDARI YA MTWARA

	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia	Ongezeko la Dola 2.134/Tani	Ongezeko la Dola 27.229/Tani	----
Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (BPS premiums)	Ongezeko la Dola 2.600/Tani	Ongezeko la Dola 26.100/Tani	----

**JEDWALI D: BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA DUNIA ZILIZOTUMIKA  
KUKOKOTOA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI**

	<b>Bandari</b>	<b>Petroli</b>	<b>Dizeli</b>	<b>Mafuta ya Taa</b>
<b>Mafuta yalipokelewa mwezi wa:</b>	<b>DSM</b>	Februari 2019	Februari 2019	Februari 2019
	<b>Tanga</b>	Februari 2019	Februari 2019	Desemba 2018
	<b>Mtwara</b>	Februari 2019	Februari 2019	----
<b>Wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia kwa mwezi:</b>	<b>DSM</b>	Januari 2019	Januari 2019	Januari 2019
	<b>Tanga</b>	Januari 2019	Januari 2019	Novemba 2019
	<b>Mtwara</b>	Januari 2019	Januari 2019	Januari 2019
<b>Wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia kwa miezi inayoonekana hapo juu inalinganishwa na wastani wa bei za mwezi:</b>	<b>DSM</b>	Desemba 2018	Desemba 2018	Desemba 2018
	<b>Tanga</b>	Novemba 2018	Novemba 2018	----
	<b>Mtwara</b>	Desemba 2018	Desemba 2018	----

**Nzinyangwa E. Mchany  
KAIMU MKURUGENZI MKUU  
EWURA**